

## **KILIMO CHA BINZARI**

### **Utangulizi**

Jina la kitalaam ni *Curcuma domestica* na kwa kiingereza ni **turmeric**. Zao hili asili yake ni Mashariki ya Mbali, na linalimwa zaidi katika mkoa wa Tanga, Kagera, Kilimanjaro, Morogoro na Zanzibar.

### **Matumizi**

Binzari hutumika kwa mapishi ya nyama, samaki na mapishi mengine kwa kuweka rangi yake ya njano. Hutumika zaidi na nchi za mashariki kama India; nchi za Ulaya hutumia kidogo sana.

### **Uzalishaji**

- **Hali ya hewa**

Humea vizuri maeneo yenye kiasi cha joto la nyuzi 24-26 za sentigredi na huzalishwa maeneo ya mwambao.

- **Udongo**

Udongo wenye rutuba na unaopitisha maji na usio na mawe au changarawe. Mahitaji ya mvua ni milimita 1200-2000 kwa mwaka. Epuka kusimama kwa maji shambani. Umwagiliaji unaweza kufanywa endapo maji hayatoshelezi. Binzari inafanya vizuri ikipandwa sehemu ya uwazi. Ingawa pia inaweza kuchanganywa na mazao mengine kama minazi.

- **Uchaguzi wa mbegu**

Mbegu zinazotumika hapa nchini ni za kienyeji bado. Tunguu kubwa zenye ukubwa

wa sm 2.5 hadi sm 3 hutumika kama mbegu. Kiasi cha tani 1.7 za vipando huhitajika kwa hekta. Tunguu za kupandwa zisihifadhiwe kwa zaidi ya mwezi mmoja kabla ya kupanda.

- **Nafasi ya upandaji**

Nafasi ya kupanda ni sm 30-45 kati ya mmea na mmea.

- **Mahitaji ya mbolea**

Matumizi ya mbolea hapa Tanzania si makubwa katika kilimo cha viungo. Tafiti zimeonesha kuwa binzari hazioneshi kufanya vizuri kwenye mbolea za viwandani. Mbolea za samadi zinaweza kutumika.

### **Uvunaji**

Uvunaji hufanywa kwa kutumia majembe au uma. Binzari huvunwa wakati majani yamegeuka rangi na kuwa njano au kahawia. Binzari isiyo na kambamba huvunwa kipindi cha miezi sita toka kupandwa na miezi 18 hadi 21 kwa binzari iliyokomaa kutegemeana na mahitaji ya soko.

Mavuno ya tani 7 hupatikana endapo binzari ikipandwa peke yake. Mavuno hupungua kiasi binzari ikipandwa mchanganyiko na mazao

mengine kwa mfano mavuno ya tani 4.8 kwa hekta yatapatikana binzari ikipandwa na minazi.

### **Utayarishaji**

.Kabla ya kuhifadhiwa binzari huchemshwa, huanikwa juani kisha hutwangwa/husagwa.

### **Mashambulizi ya wadudu na magonjwa**

Tatizo kubwa ni ugonjwa wa ukungu unaosababishwa na vimelea vinavyoitwa *Colletotrichum sp. na Glomerella cingulata*. Dalili ni madoa ya kahawia kwenye majani ambayo husambaa na kisha jani hukauka. Magonjwa haya yanaweza kudhibitiwa kwa kupiga dawa za ukungu kama Dithane M-45 kila baada ya wiki mbili.

### **Masoko**

Soko la binzari linapatikana ndani na nje ya nchi. Bei ya ndani ni kati ya Sh 350-600/- kwa kilo. Zao hili huuzwa katika nchi za Uganda, Kenya, Uingereza, Ujerumani, Mashariki ya Kati, n.k.

### **Ushauri**

Wakulima wanashauriwa kukausha binzari kwa uangalifu ili kutoharibu ubora wake.

### **Kwa taarifa zaidi wasiliana na :**

Sehemu ya Uinujaji Mazao,  
Wizara ya Kilimo Chakula  
na Ushirika,  
S.L.P. 9192,  
**DAR ES SALAAM.**

Simu: 022 2864899

Fax : 022 2864899/2862077

E-mail: [cps@kilimo.go.tz](mailto:cps@kilimo.go.tz)